# Kuzuia Wizi wa Magari

Kuchukua tahadhari na hatua za kuimarisha usalama kunaweza kupunguza uwezekano wa kuathiriwa na wizi wa magari. Vidokezo vilivyoorodheshwa hapa chini vinaweza kukusaidia kufanya gari lako kuwa lengo lisilovutia kwa wezi wa magari.

## Tahadhali

- Mara zote pandisha vioo vya madirisha, funga milango na uchukue ufunguo wako, hata kama utatoka kwa muda mfupi tu.
- Kamwe usiliache gari lako bila uangalizi.
- Egesha gari lako kwenye eneo linaloonekana vizuri.
- Kamwe usifiche seti ya pili ya funguo ndani ya gari au usiiache kwenye gari lako.
- Egesha kwenye sehemu yenye uangalizi, inapowezekana, kwani kufanya hivyo kunaongeza uwezekano mkubwa zaidi watu kuona.
- Kama una karakana itumie kama maegesho mbadala katika njia yako binafsi.
- Funga mlango wa karakana pamoja na gari lako.
- Usiache hati miliki ndani ya gari.

## Vifaa

- **Breki ya Dharura** - Hukatiza mfumo wa umeme, mafuta au kuwasha.
- **Kufuli ya Usukani** - Huzuia usukani usigeuzwe zaidi ya nyuzi chache; huonekana toka nje ya gari.
- **Kibanio** – Huzuia safu wima ya usukani kuchomolewa.
- **Kufuli la Breki** – Huzuia breki isihusike kuondoa klachi, gea na wenzo pamoja kutoka kwenye maegesho.
- **Uchoraji wa asidi** - Kuandika namba ya VIN kwa asidi kwenye kioo cha gari kunaweza kuifanya iwe na thamani ndogo kwa wezi.

*Wizi mwingi wa magari hufanyika usiku au alfajiri, na zaidi ya nusu hufanyika katika maeneo ya makazi ikiwemo kwenye majengo ya ghorofa.*

# Kuzuia Uporaji wa Magari

Uporaji wa magari ni uhalifu wa fursa; magari ni shabaha rahisi na mara nyingi huwa na mali inayovutia wezi. Sehemu kubwa za maegesho na maeneo yenye maegesho mengi ya barabarani yenaweza kuwa shabaha kuu ya wizi. Tumia vidokezo rahisi, vya bei nafuu vilivyo hapa hapa chini ili kupunguza hatari yako.

## Tahadhali

- Usiache kitu chochote katika mwonekano wa wazi ndani ya gari lako.
- Egesha gari katika maeneo yanayoonekana vizuri na mwanga wa kutosha.
- Pandisha vioo vya vya madirisha na ufunge milango.
- Weka vitu kwenye kasha lako kabla ya kufika kwenye kituo chako.
- Hifadhi kasha, mfuniko wa mlango, masanduku ya vifaa vya kupachika kitanda na kanopi.

## Ondoa Vitu Hivi

- Vifungua milango ya karakana
- Vifaa vya kielektroniki (komputa mpakato, simu za mkononi)
- Mizigo/mabegi
- Nyaraka/vyombo vya fedha
- Fedha taslimu
- Silaha za moto
- Barua
- Mkoba/Pochi

ALBUQUERQUE POLICE

ONE ALBUQUERQUE APD